TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Kumb na: Taro /P/2022/ A13 **: Swahili Version:** Tarehe: 13 Mei 2022

**MTAZAMO WA KISHERIA KUHUSU MWENENDO WA KUFUNGIA NYIMBO UNAOFANYWA NA BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA) NA TCRA**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Tangu kupitishwa kwa Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za mwaka 2018, tumeshuhudia nyimbo nyingi za muziki wa kizazi kipya kufungiwa na **Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)** wakishirikiana na **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communication Regulatory Authority-TCRA)**. Mnamo tarehe 6 Mei 2022, Gazeti maarufu nchi **(MWANANCHI)** kupitia tovuti yake lilichapisha taarifa iliyoandikwa na Mwandishi **(Nasra Abdallah)** kama ilivyonukuliwa *"Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imepiga marufuku vyombo vya utangazaji na mitandao ya kijamii kutoonyesha wimbo wa "Mtasubiri" ulioimbwa na msanii Nasib Abdul maarufu kwa jina la Diamond Platnumz akimshirikisha msanii mwenzake Zuhura Othman (Zuchu)…".*

Sababu za kufungia video hiyo ni kuwa kipande kinachoonyesha kanisani kimeleta ukakasi miongoni mwa waumini wa madhehebu ya dini na kuleta hisia kwamba ni dharau juu ya dini/madhehebu Fulani. Mamlaka zimeagiza video hiyo kurekebishwa ndio iendelee kutumika.

Taarifa hiyo imesababisha sintofahamu kubwa miongoni mwa wasanii wa muziki na jamii kiujumla. Sintofahamu hiyo imejikita katika kuhoji uhalali wa maamuzi hayo yaliyofanywa na TCRA. Ambapo TARO tumeamua kulizungumzia suala hili kwa kujikita katika sheria kama ifuatavyo:-

**HOJA ZA KISHERIA**

**Je sheria imetoa utaratibu wowote unaozuia msanii kupata hasara kutokana na kazi yake kufungiwa?**

A. Kwa mujibu wa kanuni ya **25(1)** ya **kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa Mwaka 2018**, zinaelekeza kuwa *"Hakuna kazi ya sanaa itakayopelekwa sokoni ama kwa walaji,kabla ya kupewa kibali cha kudhibitisha kuwa maudhui yamezingatia maadili".**(ITHIBATI YA MAADILI)***
B. Kwa mujibu wa kanuni ya **25(7)** ya **kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa Mwaka 2018**, zinaelekeza kuwa *" Endapo kazi yoyote ya sanaa itabainika kwenda kinyume na masharti ya maadili kwa mujibu wa kanuni hizi, wahusika wote katika utayarishaji na utangazaji wa kazi hiyo watakua wametenda kosa"*
C. Kwa mujibu wa kanuni ya **25(8)** ya **kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa Mwaka 2018**, zinaelekeza kuwa *"Baraza litachukua hatua zifuatazo kwa utekelezaji wa masharti ya kanuni hii:- (a) Litafungia kazi husika mapema iwezekanavyo (b) msanii na mzalishaji aliyefanya kazi hiyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu na kanuni hizi"*
D. Kwa mujibu wa kanuni ya **26(1)** ya **kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa Mwaka 2018**, zinaelekeza kuwa *" Vyombo vya habari havitaruhusiwa kupokea wala kurusha kazi za sanaa ambazo hazitakuwa na **ithibati ya maadili** kutoka Baraza"* .Adhabu ya kukiuka kanuni hii ni faini isiyopungua milioni moja.

**Je ni sababu gani za kiimani (kidini) zinaweza kusababisha kazi ya sanaa (nyimbo) kufungiwa kupigwa kwenye vyombo vya utangazaji na mitandao ya kijamii?**

A. Kwa mujibu wa Jedwali la Tatu la kanuni iitwayo **Electronic and Postal Communications (Online Content).Gn. No. 538 of 2020** limetoa orodha ya maudhui yanayokatwaza na sheria. Kipengele cha **7(a)** cha Jedwali hilo kinaelezea **Heshima kwa dini** na **Imani za watu.** Kipengele hicho kinakataza maudhui yaliyobeba au kuhamasisha maudhi, kudhalilisha/kudharaulisha, kutukana, kuleta mzaha au kukiuka dini yoyote au utaratibu wake wa kiimani au utakatifu wake au vitabu vyake vitakatifu au kuingilia uhuru wa mtu wa kuabudu dini yake kwa kutumia fujo au vitisho.

**Je TCRA wanayo mamlaka ya kufungia nyimbo kupigwa kwenye vyombo vya utangazaji na mitandao ya kijamii?**

A. Kwa mujibu wa kifungu cha **27(1)** cha sheria iitwayo **Tanzania Communication Regulatory Authority Act. No.13 of 2003** kimeipa mamlaka Kamati ya Maudhui ya **TCRA** kudhibiti na kusimamia maudhui yanayotangazwa**.**
B. Kwa mujibu wa kanuni ya **19(b)** ya kanuni ziitwazo **Electronic and Postal Communications (Online Content).Gn. No. 538 of 2020** zinaipa mamlaka **TCRA** kutoa amri ya kuondolewa au kuzuia upatikanaji kwenye vyombo vya utangazaji na mitandao ya kijamii maudhui yanayokinzana na kanuni tajwa.
C. Kwa mujibu wa kanuni ya **6** ya kanuni ziitwazo **Electronic and Postal Communications (Radio and Television Broadcasting Content)(Amendment) Regulations 2020. Gn. No. 486 of 2020** ambazo zimerekebisha kanuni ya **45** ya kanuni ziitwazo **Electronic and Postal Communications (Radio and Television Broadcasting Content) Regulations 2018, Gn.No. 134 of 2018,** zinaipa mamlaka **TCRA** kutoa amri ya kuondolewa kwenye vyombo vya utangazaji (Runinga na redio) maudhui yanayokinzana na kanuni tajwa.



TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

**Je msanii ana haki ya kusikilizwa na kujitetea kabla ya kufungiwa kwa kazi yake ya sanaa (Nyimbo) na BASATA au TCRA?**

**A.** Kwa mujibu wa ibara ya **13(6)(a)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(1977)** kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, inaelekeza kuwa *"Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya **kusikilizwa kwa ukamilifu,** na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya sheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika"*

**Je msanii akihisi ameonewa kutokana na maamuzi ya BASATA/TCRA kufungia nyimbo yake kupigwa kwenye vyombo vya utangazaji na mitandao ya kijamii anaweza kutafuta haki yake sehemu nyingine kisheria?**

A. Kwa mujibu wa kifungu cha **22** cha sheria iitwayo **Written Laws (Miscellaneous Amendment)(No.5) Act, 2019** kimerekebisha sheria ya sanaa iitwayo **Nationa Arts Act. No.23 of 1984** na kuongeza kifungu kipya cha **15A.** Kwa mujibu wa kifungu hicho kipya cha **15A(1)** kinaeleza kuwa mtu yeyote ambaye ameumizwa na maamuzi ya Baraza la Sanaa la Taifa(BASATA) anaweza kukata rufaa ndani ya siku 30 dhidi ya maamuzi hayo kwenda kwa waziri husika.

B. Kwa mujibu wa kifungu cha **36(1)** cha sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania **(Tanzania Communication Regulatory Authority Act. No.13 of 2003)** iliyofanyiwa marekebisho na sheria iitwayo **Electronic and Postal Communication Act. No. 3 of 2010**, inatoa nafasi ya mtu yeyote asiyeridhishwa na maamuzi ya **TCRA** kukata rufaa dhidi ya maamuzi hayo kwenye Baraza la Ushindani huria **(Fair Competition Tribunal).**

**<u>HITIMISHO</u>**

Kutokana na kanuni za Baraza la Sanaa zilizopo sasa zinaingilia na kubana uhuru wa kujieleza katika kazi za kibunifu za sanaa, TARO tunawasihi na kuwakumbusha wasanii kushirikisha wanasheria katika maandalizi na uendeshaji wa kazi zao za sanaa ili kuepuka hasara zisizo za lazima kwa kipindi hiki ambapo sheria hizo hazijafanyiwa marekebisho. TARO tunawasihi, kuwakumbusha na kuwataka **BASATA** na **TCRA** kuheshimu katiba ya **nchi** kwa kuheshimu **haki ya kusikilizwa** kwa wasanii kabla ya kufanya maamuzi ya kufungia kazi zao. Pia ni jukumu la **BASATA** na **TCRA** kuwaeleza wasanii na umma kwa ujumla kuhusu haki yao ya kukata rufaa, endapo hawataridhika na maamuzi ya kufungiwa kwa kazi zao. Maamuzi ya kufungia kazi za wasanii yasitekelezwe mpaka pale rufaa itakaposikilizwa au muda wa rufaa utakapopita ili kuzuia mashambulio haya makali ya kiuchumi kwa wasanii.

**ASANTENI**

MUNGU AIBARIKI TANZANIA, MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA

(Kazi iendelee)

**Wako katika kujenga Taifa**

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**

**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**